ISO 9001:2015 Certified

The Regulator

JARIDA LA KILA ROBO MWAKA LA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

Linatolewa bure

ISSN: 0856 - 8030 TOLEO NA. 2/2024 APRILI - JUNI 2024



# Uvumbuzi kwa Maendeleo Endelevu

# Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)







**Soma kujisajili**

Jarida hili linakuwezesha kupitia na kupata stadi mpya na pia kupanua mtandao wako wa watu wenye weledi kama wewe. Kupata nakala za bure za jarida hili na kuwasilisha maoni, tuma barua pepe kwa

regulator.magazine@tcra.go.tz | barua@tcra.go.tz

Tunakaribisha maoni na hoja kutoka kwa wasomaji wetu. Kwa maelezo zaidi tafadhali piga simu ya bure kwenye namba ya wateja wa TCRA, ambayo ni **0800008272.**

ISSN: 0856 - 8030
NAMBA YA USAJILI: 00000115
Na. 2/2024. APRILI - JUNI, 2024

# The Regulator

Hili ni toleo la Kiswahili la jarida la The Regulator, linalotolewa mara nne kwa mwaka na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). TCRA ni taasisi ya serikali inayosimamia mawasiliano ya kielektroniki na posta nchini. Jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka.

## Sheria Na. 12 ya mwaka 2003 iliyoanzisha TCRA inaipa Mamlaka wajibu katika majukumu yafuatayo:

1. Kukuza ushindani bora na uchumi wenye tija;
2. Kulinda maslahi ya watumiaji;
3. Kulinda mitaji ya Watoa Huduma wenye ufanisi;
4. Kukuza upatikanaji wa huduma zinazodhibitiwa kwa watumiaji wote wakiwamo wenye kipato kidogo, walioko vijijini na watumiaji walio na walioko katika mazingira magumu;
5. Kuimarisha Elimu kwa Umma, uelewa na ufahamu wa huduma zinazosimamiwa na TCRA, ikiwa ni pamoja na:
   (i) Haki na wajibu wa watumiaji na watoa huduma zinazosimamiwa;
   (ii) Namna ya kuwasilisha malalamiko na migogoro na utaratibu wa utatuzi wake; na
   (iii) Kazi na majukumu ya Mamlaka kwa kuzingatia umuhimu wa kulinda na kutunza mazingira.

## MKAKATI WA TCRA 2021/22-2025/26 NA MALENGO YA KIMKAKATI

Mamlaka imeandaa Malengo mbalimbali ili kufikia maono yake katika kukabiliana na mambo muhimu kama yalivyobainishwa katika uchambuzi wa hali halisi ya kisekta. Malengo hayo ni:-

1. Kukuza miundombinu na huduma za mawasiliano ya kielektroni na posta yenye usalama, ufanisi na imara;
2. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya kielektroni na posta zenye ubora na unafuu;
3. Kuimarisha ubunifu wa huduma zinazodhibitiwa, uandaaji wa maudhui ya ndani na ujanibishaji;
4. Kuimarisha ufanisi wa huduma zinazodhibitiwa na kuwalinda wadau; na
5. Kuimarisha uwezo wa taasisi.

## MATOKEO YA MKAKATI

1. Kupatikana kwa huduma za mawasiliano za uhakika na salama;
2. Kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za mawasiliano zilizo bora na nafuu;
3. Jamii yenye kuzalisha na kutumia maudhui ya ndani;
4. Kukua kwa ufanisi wa sekta ya mawasiliano na uzingatiaji wa sheria, kanuni, miongozo, kanuni ndogo na viwango kwa wadau wa sekta ya mawasiliano; na
5. Kuongezeka kwa ufanisi wa kiutendaji wa taasisi.

## SERA YA UBORA

Kutokana na nguvu za kisheria za kusimamia sekta za Mawasiliano ya Kielektroni na Posta Tanzania, TCRA imejidhatiti kuweka mazingira mazuri kwa Wenye Leseni kwa kutoa rasilimali, kudumisha na kuendelea kuboresha Mfumo wa Usimamizi wa Ubora ili kuhakikisha utoaji wa huduma bora na nafuu kwa watumiaji ili kukidhi matakwa ya Sheria na ya kiudhibiti.

## BODI YA WAHARIRI

**Mwenyekiti**
Mhandisi. Mwesigwa Felician

**Katibu**
Bw. Rolf Kibaja

**Wajumbe**
Bw. Semu Mwakyanjala (Mratibu)
Dkt. Philip Filikunjombe
Dkt. Peter Kihogo
Bw. Peter Lyimo
Bw. Robin Ulikaye
Bw. Abel John
Bi. Vitalia Kidabulo
Bw. Alpha Wawa

**Mhariri Uzalishaji**
Bw. Isaac Mruma

**Anwani ya ofisi za uhariri**
Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma,
S.L.P 474,
Postikodi 14414 Dar es Salaam.
Simu: +255 784558270, +255 784558271.
Barua pepe: regulator.magazine@tcra.go.tz; dg@tcra.go.tz
@tcra_tanzania

# Yaliyomo

04 Ujumbe wa Mkurugenzi Mkuu



06 Taasisi za usimamizi na uvumbuzi



08 Uvumbuzi nguzo kuu Mkakati kidijitali





11 Vilabu vya Kidijiti Kuongoza Ubunifu Mashuleni




15 Upimaji viwango vya mawasiliano wa pamoja waonesha tija




19 Takwimu sekta ya Mawasiliano



BARUA YA MHARIRI

# Uvumbuzi kwa Maendeleo Endelevu

Kuna matukio matatu yanayohusiana na mawasiliano, ambayo yanaangukia kila robo mwaka ya Aprili hadi Juni.

Ni kipindi ambacho Bunge linakaa kupitisha makadirio ya wizara mbalimbali, ikiwemo ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (HMTH). Vilevile kila Alhamisi ya nne ya mwisho wa Aprili, dunia inaadhimisha Siku ya Wasichana na TEHAMA Ulimwenguni.

Tarehe 17 Mei ni siku ya Mawasiliano ya Simu na Jamiihabari, yaani inayotumia mifumo ya kompyuta na data. Mkataba ulioanzisha Umoja wa Mawasiliano Kimataifa, ambao baadae ukawa Shirika la Mawasiliano Ulimwenguni, ulisainiwa tarehe hiyo.

Siku ya Wasichana na TEHAMA duniani imetengwa ili kuhimiza wanafunzi wasichana kupendelea masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati.

Masomo haya ni muhimu kuelewa na kuendeleza stadi za masuala ya kidijiti. Pia yanajenga msingi wa utaalamu kwenye TEHAMA na mawasiliano kwa ujumla, ambayo ni muwezeshaji wa sekta nyingine.

Serikali ya Tanzania inatekeleza mkakati wa kutumia TEHAMA kwenye sekta zote ili kujenga uchumi wa kidijiti na wa buluu.

Toleo hili limejielekeza kwenye uvumbuzi au ubunifu; mojawapo ya nguzo za uchumi wa kidijiti.

Kaulimbiu ya Siku ya Wasichana na TEHAMA ilikuwa Uongozi, ukijumuisha ule utakaoiwezesha Tanzania kufikia malengo yake ya kujenga jamii yenye uelewa, upeo mkubwa na stadi za kidijiti. Kumbukumbu ya tarehe 17 Mei ziliongozwa na ujumbe wa Uvumbuzi kwa Maendeleo Endelevu.

Hotuba ya Waziri wa HMTH, Mhe. Nape M. Nnauye Bungeni inaelezea mipango ya kuanzisha maeneo ya ubunifu wilayani. Pamoja na taarifa kuhusu hayo, tumepitia mkakati wa Mpango wa miaka 10 wa Tanzania ya Kidijiti (2024-2034) na Sera ya Taifa ya TEHAMA.

Tumeonesha mchango wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)_katika kuendeleza uvumbuzi na kuwezesha vipaumbele vya serikali kwenye sekta.



UJUMBE WA MKURUGENZI MKUU

# Kuimarisha uchumi wa kidijiti



Dkt. Jabiri K. Bakari, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA

Ubunifu wa kidijiti ni nguzo muhimu kwenye uchumi wa kidijiti ili kuendana na maendeleo ya kiuchumi na maendeleo ya kimataifa.

Katika mazingira ya kisasa ya kidijitali yanayobadilika kwa kasi, ubunifu huwezesha kuzitambua fursa zilizopo na kutatua changamoto zinazoikabili jamii na kutoa majawabu yenye tija kupitia TEHAMA.

Kauli mbiu ya mwaka huu ni wito wa kuwepo jitihada za makusudi za kuweka mazingira ya kuchagiza ubunifu wa kidijiti nchini kuendana na kasi ya maendeleo ya Dunia ili kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (UN ifikapo mwaka 2030.

Kwa kutambua umuhimu wa Ubunifu, TCRA kwa kushirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) inaunga mkono kazi za ubunifu wa kiteknolojia kwa kutoa rasilimali za mawasiliano. Hizi ni pamoja na rasilimali za namba, masafa, na Kikoa cha Dot. Zinatolewa bure kwa wabunifu mbalimbali ambao wanahitaji kujaribu huduma zao za kibunifu kwa kipindi cha miezi mitatu (siku 90) ili kuwawezesha na kuinua mawazo yao ya bunifu mbalimbali.

Kwa mfano TCRA imetenga rasilimali namba *146*XX ambayo inatolewa bure kwa majaribio ya wabunifu.

TCRA inaendelea kuangalia na kuunda mazingira yanayoweza kusaidia zaidi mzunguko wa maisha ya kampuni changa kuelekea kuwa biashara huru zenye mafanikio.

Aidha, katika kuweka mazingira ya ubunifu kwa wanafunzi TCRA inaratibu klabu za kidijiti kwa shule za awali, za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu nchini. Madhumuni ni kuhimiza wanafunzi kujifunza na kuyapenda masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati ambayo yana umuhimu mkubwa katika kukuza ujuzi wa uchumi wa kidijiti unaohitajika ili kufanikiwa kujenga Tanzania ya kidijiti. Vile vile TCRA inashirikiana na Watoa Huduma katika kuwawezesha wabunifu kufanikisha bunifu zao kupitia mifumo ya TEHAMA

TCRA inatambua mchango wa watoa huduma na wadau wote wa sekta ya mawasiliano na hivyo inahimiza kuendelea kuwekeza kwenye miundombinu ya mawasiliano na TEHAMA na kutoa huduma mbalimbali za TEHAMA. Hii inakusudiwa kuweka miundombinu na mazingira imara ya mawasiliano Tanzania ili kuwezesha mabadiliko ya kidijiti na kuchochea ubunifu nchini.

> "
> Tanzania, kupitia TCRA, inashiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ya TEHAMA ulimwenguni. Ni mjumbe wa Bodi ya Muungano wa Ubunifu na Ujasiriamali kwa Maendeleo ya Kidijiti duniani.
>
> **Dkt. Jabiri K. Bakari**

Vilevile Tanzania ni miongoni mwa nchi sita za Afrika zenye vituo vya Shirika la Mawasiliano Ulimwenguni (ITU) vinavyolenga kuharakisha matumizi ya mitandao. Nchi nyingine ni  Kenya, Malawi, Zimbabwe, Gabon na Senegal. Vituo hivi vitawezesha vyuo vikuu na taasisi za utafiti kupata huduma na vifaa kwa njia ya mtandao, kutumia nafasi ya kidijiti katika kubuni, kujaribu na kutekeleza suluhisho za kidijiti.

Kwa mujibu wa ITU, teknolojia za kidijitali zinaweza kusaidia kufikia asilimia 70 ya malengo, chini ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ifikapo mwaka 2030.

## Wanahabari mtandaoni wakumbushwa kuwajibika kimaadili



*Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) amewataka waandishi mitandaoni kutumia mitandao ya kijamii kama nyenzo muhimu ya kuleta maendeleo na kuchochea mabadiliko chanya.*

Akifungua kongamano la mwaka 2024 la Jumuiya ya Wanahabari ya Mitandao ya Kijamii Tanzania (JUMIKITA) Mei 2024 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ameonya dhidi ya matumizi mabaya ya mitandao ambayo yanaweza kusababisha athari mbaya kijamii.

"Mitandao ina nguvu ya kubadili jamii yetu kuwa jamii bora. Tuitumie kwa njia inayofaa kuleta maendeleo," alisisitiza.

Wanahabari, wakiwemo wa mitandaoni wanawajibika kuhakikisha kwamba wanatumia majukwaa yao kuelimisha na kuhimiza maendeleo badala ya kuzua taharuki kwa jamii, aliongeza.

Mwenyekiti wa JUMIKITA, Shabani Omary Matwebe alisema JUMIKITA inadhamiria kuhakikisha mitandao ya kijamii inatumika kama kichocheo cha maendeleo Tanzania.

## TCRA yahimiza weledi uandishi mitandaoni

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inashirikiana na JUMIKITA kukabiliana na kasoro zinazojitokeza kwenye uandishi mitandaoni. Ushirikiano huu utahusisha pia elimu kuhusu kanuni za maudhui ya utangazaji.

Aidha, Kamati ya Maudhui ya TCRA inakutana mara kwa mara namara na watoa huduma za maudhui mitandaoni na kujadili namna ya kuzingatia kanuni.

Utafiti mdogo uliofanywa na TCRA mwaka wa fedha 2021/22 na 2022/2023 ulionesha kuwa vyombo vingi vya habari mtandaoni vinakiuka kanuni za kumlinda mtoto, kulinda wahanga wa ukatili wa kijinsia na vinatumia lugha mbaya.

Vilevile kuna tatizo la kutokuzingatia mizania wakati wa kutoa habari, kuweka maoni binafsi kwenye maudhui na kuhamasisha uchochezi na vurugu.

Maeneo yanayokiukwa mara kwa mara kwenye utangazaji yako kwenye kanuni za utangazaji wa redio na televisheni na kanuni za maudhui mtandaoni.

Kanuni za maudhui yanayohusu watoto na wahanga wa makosa ya kijinsia.

Mtoa huduma hatakiwi kutoa utambulisho wa mhanga wa matendo maovu au ukatili wa kijinsia isipokua tu pale ambapo mhanga ataridhia kuwa atambulishwe; na akubali kwa maandishi.

Mtoa huduma hatakiwi kutoa utambulisho wa mhanga wa matendo ya maovu au ukatili wa kijinsia isipokua tu pale ambapo mhanga ataridhia kuwa atambulishwe; na akubali kwa maandishi.

Ziko kanuni nyingi zinamzungumzia mtoto. Vyombo vy utangazaji visitoe utambulisho wa watoto ambao ni wahanga wa ubakaji au uhalifu mwingine. Hii ni pamoja na kutowasumbua au kuwadhuru watoto. Vilevile msisitizo uko kwenye kuwalinda dhidi ya maudhui hasi yanayoweza kuigwa.

Kutokutoa maudhi yanayoonesha matumizi ya nguvu, na kuzingatia muda wa kutoa vipindi na maudhui ya rika zote pia ni njia ya kumlinda mtoto.

Kanuni kuhusu uwasilishaji wa habari na matukio, utoaji maoni binafsi na kuhusu lugha zimelenga kurekebisha ukiukwaji huu. Suala la matumizi sahihi ya lugha sanifu, sahihi na kamilifu liko kwenye kanuni nyingi.

# Taasisi za usimamizi na uvumbuzi

Na Mwandishi wetu

Kwa ujumla wake, bidhaa na huduma za mawasiliano ni ama matokeo ya uvumbuzi au zinawezeshwa na uvumbuzi. Uvumbuzi unawezesha kuboresha bidhaa na huduma.

Kwa mfano ugunduzi wa masafa ya redio umewezesha kuyatenganisha kwa matumizi mbalimbali na tofauti.

Ndani ya matumizi hayo kuna uvumbuzi wa ama vifaa vinavyowezesha matumizi yake na huduma zinazotokana na matumizi hayo.

Uvumbuzi ni shughuli endelevu, inayoweza kufanyika kwenye aina moja ya huduma na bidhaa au aina nyingi.

Nyingi za bidhaa za mawasiliano zinazoingia Tanzania na kutumiwa ni matokeo ya wavumbuzi wa shughuli za kidijitali. Watafiti na wavumbuzi wanawezesha kupatikana bidhaa na huduma mpya zinazoingia sokoni kwa kasi.

Mfano wa kila siku wa uvumbuzi ni kwenye simu za mkononi, ambazo zimeendelea kuwa tofauti kwa umbo, ukubwa na uwezo wa vijenzi na vifaa vinavyo wezesha matumizi, kama vile vya kuchajia au kusikilizia.

Kwa muda mrefu sasa, wasimamizi wa huduma za mawasiliano wamekuwa wanatoa leseni kwa utoaji huduma kupitia vifaa vilivyokubalika kiviwango kimataifa.

Miaka ya hivi karibuni imeibua suala la uwezekano wa wasimamizi pia kupanua wigo wao wa usimamizi na kuona namna ya kuchochea ukuaji wa huduma mpya.

Wengi sasa wanasimamia uvumbuzi unaokusudia kuingiza huduma mpya kwenye soko. Wamewezesha kuwepo muda wa majaribio, wanasimamia shughuli za wavumbuzi na wanaotumia kanuni na miongozo ya usimamizi.

Lengo ni kuhakikisha kwamba bidhaa mpya zinazotokana na uvumbuzi haziathiri shughuli zinazofanywa na watoa huduma wenye leseni ambao wanatoa huduma zinazokusudiwa kuingizwa sokoni na wavumbuzi.

Wavumbuzi wanatumia raslimali za mawasiliano zilizoko na zinazotolewa bure kwao.



Wasimamizi wanataka kuhakikisha kwamba shughuli za wavumbuzi na kampuni changa zinazofanya, au zinazotokana na uvumbuzi haziingilii au kushindana na shughuli zinazofanywa na watoa huduma wenye leseni zinazolipiwa.

Lakini pia lengo ni kuhakikisha uvumbuzi na matokeo yake haviathiri shughuli za usimamizi.

Hii ni pamoja kuhakikisha kuwa viwango vya kikanuni vinazingatiwa na watumiaji wanalindwa dhidi ya huduma zinazovumbuliwa.




Mfumo wa usimamizi wa uvumbuzi unatoa motisha kwa wajasiriamali au kampuni changa ili kuwezesha kuanzishwa huduma mpya na za aina mbalimbali.

Usimamizi wa uvumbuzi unawezesha wavumbuzi kuingia kirahisi kwenye mfumo wa leseni na utoaji huduma. Ni rahisi zaidi kwa wanaofanikiwa kupata leseni za huduma kwa kuwa shughuli zao zimejaribiwa na kufanyika chini ya usimamizi.

Usimamizi wa uvumbuzi unahitaji imani za pande zote mbili, imani ya wavumbuzi kwa msimamizi kwamba taarifa zao hazitatumika kiusimamizi na kuwatendea kinyume na watoa huduma wengine ambao hawakupita chini ya jicho la karibu la msimamizi.

Wasimamizi wanafuatilia uvumbuzi wowote kwani unaweza kutoa au kuleta mabadiliko yatakayohitaji marekebisho au mabadiliko ya mfumo wa usimamizi.

Ingawaje usimamizi wa uvumbuzi kuna matatizo yanayojitokeza, uvumbuzi unaosimamiwa unawezesha wasimamizi kuona vihatarishi vya uvumbuzi na kuchukua hatua stahiki.

Changamoto mojawapo ya usimamizi wa uvumbuzi ni pale unapohusisha wasimamizi zaidi ya mmoja. Kwa mfano mvumbuzi anapotaka kutoa huduma ambazo zinahitaji uzingatiaji wa kanuni zinazosimamiwa na taasisi tofauti. Mfano ni huduma za fedha, ambazo ndani kuna TCRA inayotoa namba na misimbi ya kutumika kwenye miamala na Benki Kuu ya Tanzania inayosimamia sekta ya fedha.

Vilevile Tanzania ina taasisi mahsusi kwa utafiti, ambayo inakuza matumizi mbalimbali ya kiteknolojia. Hii ni Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Tanzania (COSTECH). TCRA inashirikiana na Tume hii katika mpango wa kukuza uvumbuzi.

Taasisi hizi zina majukumu ya kuratibu na kukuza shughuli za mawasiliano, utafiti na maendeleo ya teknolojia Tanzania. Waombaji wa raslimali za mawasiliano kwa kujaribu uvumbuzi wao au miradi yao wanatakiwa kwanza kupata idhini ya COSTECH.

Vilevile, matumizi ya huduma zinazotokana na miradi ya uvumbuzi inayowasilishwa na kuwezeshwa na TCRA yanabidi kuidhinishwa na wasimamizi wa sekta husika, kama vile usafiri na nishati.

> Ubunifu wa kidijiti wenye tija ni muhimu ili kuwa na huduma za TEHAMA zilizoboreshwa zinazolenga kutatua matatizo mbalimbali.

Serikali ya Tanzania inaamini katika kuendeleza mazingira yanayosisitiza ubunifu na ujasiriamali. Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe Nape M. Nnauye alisema tarehe 17 Mei, siku ya kuadhimisha kuanzishwa kwa Shirika la Mawasiliano Ulimwenguni kuwa uvumbuzi unaweza kutatua changamoto za kimawasiliano zinazokabili makundi ya watu yaliyotengwa kihuduma.

Mipango ya kuunga mkono kuanzisha biashara ndogo, hasa zile zinazojikita katika kutatua changamoto za ndani, ni sehemu muhimu ya mkakati wetu wa kukuza ukuaji wa kiuchumi kwa njia ya ubunifu wa kidijiti, alisisitiza.

# Uvumbuzi nguzo kuu Mkakati kidijitali



-Mhe **Dkt. Samia Suluhu Hassan**
*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

Serikali imepitisha Mkakati wa Kitaifa wa Uchumi wa Kidijitali, utakaotekelezwa kati ya 2024 na 2034. ambamo utamaduni wa uvumbuzi na ubunifu wa kidijiti vimeelezwa kama msingi muhimu wa kuijenga Tanzania kiteknolojia.

Mkakati huo wenye nguzo sita unalenga kuongeza matumizi ya kidijitali kwa huduma zinazotolewa na Serikali pamoja na Sekta binafsi.Kwenye ujumbe wa uzinduzi wa Mpango huo, Rais, Dkt Samia Suluhu Hassan anasisitiza kuwa mkakati huo utafanikiwa iwapo wadau wote watajitoa kuutekeleza, na fursa zote zitafuatiliwa.

Mpango unakusudia kuweka urithi wa kidijitali ambao utathaminiwa na kuhifadhiwa kwa upendo mkubwa na vizazi vijavyo, amesema.

Wadau muhimu watashirikishwa kuandaa mfumo jumuishi utakaowezesha watu nchini kuwa na namba pekee ya utambulisho itakayofanikisha mawasiliano na miamala ya kifedha.

Kutakuwa na Jamii Namba,Jamii Malipo na Jamii data Shirikishi. Namba itakuwa ni utambuzi wa kipekee wa kila mwananchi kuanziaanapozaliwa ambapo atakuwa na akaunti ya kidijitali itakayomwezesha kupata huduma zote za kijamii, mkakati huo unaonesha.

Mfumo wa Jamii Malipo utawezesha wananchi kutumia Jamii Namba kupokea fedha na kurahisisha kufanya malipo kidijitali. Mfumo huu pia utasaidia kujenga ushirikishaji kifedha na kuongeza wigo wa mapato ya Serikali.

Mfumo wa Jamii Data Shirikishi unamwezesha mwananchi kumiliki taarifazake anapotaka na kupokea huduma mbalimbali nchini. Mfumo huu unajengwakwa ushirikiano wa Wizara, kupitiaMamlaka ya Serikali Mtandao, ambayo imehamishiwa huko siku za karibuni,na Tume ya TEHAMA.

Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ya mwaka 2016 itapitiwa upya. Uvumbuzi na ubunifu ni miongoni mwa masuala ya kipaumbele kwenye sera hiyo.

Sera mpya itaainisha Mkakati wa Kufanya Tafiti na Bunifu za TEHAMATanzania, mikakati ya matumizi ya akili mnemba na Mkakati wa Usalama Mtandaoni.

Maboresho ya Sera hiyo yatawezesha Tanzania kuwa na viwango vinavyotambulika kimataifa katika TEHAMA, na kujenga uelewa kwa wananchi wote kuhusu matumizi ya TEHAMA.

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaandaa miongozo ya usimamizi wa Sekta ya TEHAMA.

# Sera ya Taifa TEHAMA na Uvumbuzi

Na Mwandishi wetu

Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ambayo imepitiwa upya na kurekebishwa, inatambua mchango wa mazingira wezeshi ya kisera na kiusimamizi katika kukuza uvumbuzi kidijitali.

Sera hiyo inalenga kuibadili Tanzania kuwa ya kidijiti, yenye uchumi imara ambao unawezesha na kuendeleza uvumbuzi na ujasiriamali wa kidijiti. Vilevile lengo ni kuwezesha Tanzania kufikia na kupita malengo ya kikanda Afrika na kimataifa kama yalivyoainishwa kwenye Malengo ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu ifikapo 2030 na yale ya Dira ya Umoja wa Afrika 2063.

Mipango itatekelezwa kuendeleza miundombinui ya TEHAMA na kuwekeza kwenye huduma za kidijiti zenye ubunifu.

## Sera ya TEHAMA pia inagusia yafuatayo:

- Umuhimu wa kuendeleza utamaduni wa uvumbuzi na ujasiriamali. Utamaduni huu unapaswa kuwezeshwa na mipango ya kufundisha upya na kuongeza stadi za wafanyakazi ili kuongeza sifa za kitaalamu za kidijiti zinazohitajika kwenye uchumi wa kidijiti.
- Kuondoa mapengo ya kiwango cha stadi za kidijiti na pia kuweka azma ya pamoja ya ushirikiano wa wadau wote kwenye sekta ya umma na binafsi. Hii itawezesha kujenga uchumi imara wa kidijiti unaostahimili mabadiliko na unaoshirikisha wadau wengi.
- Utafiti na maendeleo, uvumbuzi na ujasiriamali kwenye TEHAMA ni muhimu ili kufikia maendeleo endelevu na ili kuiwezesha Tanzania kutumia fursa zinazojitokeza kwenye maendeleo ya teknolojia kipindi hiki cha kidijiti.
- Maendeleo ya Uchumi wa Tanzania yanaonekana kwa ukuaji wa wastani wa asilimia 6.6 ya pato la taifa ndani ya miaka 20 iliyopita. Pamoja na ukuaji huu, kuna ukuaji wa kiwango cha maendeleo ya watu ndani ya miaka 30 iliyopita. Uandikishaji watoto kwenye shule za msingi umeongezeka kutoka asilimia 51 ya watoto wanaostahili kuwa shule za msingi mwaka 1990 hadi 95 ilipofika 2023.
- Hali hii inaifanya Tanzania kuweza kuwa kitovu cha uvumbuzi na ujasiriamali kwenye kanda hii ya Afrika na kwa Afrika. Ujasiriamali na uvumbuzi wa kidijiti vinaendelea kuwa vipengele muhimu kwenye ukuaji wa uchumi wa kidijiti Tanzania na utahakikisha ukuaji endelevu wa uchumi.
- Kwa ujumla wake, uvumbuzi Tanzania uliongezeka kwa asilimia 15 kwa upande wa wenye miradi ya uvumbuzi wanaojitokeza. Kampuni zinazojitokeza kutokana na uvumbuzi zilifikia 673 mwaka 2022. Ukuaji huu umechochewa na kuongezeka upatikanaji wa teknolojia na kuchukuliwa kwake kwa matumizi na mabadiliko ya fikra na ari ya ujasiriamali, hususan miongoni mwa vijana wanaoamua kujiajiri.

**673** Kampuni changa  **15%**

Sekta ya huduma za kitaalamu na utaalamu elekezi za wajasiriamali wanaojitokeza, ikiwa ni pamoja na huduma za programu zinazotumia kompyuta inaongoza kwa asilimia **25.9**. Dar es Salaam inaongoza kama kitovu cha wavumbuzi wanajitokeza, ikiwa na asilimia **66.56** ya wajasiriamali wanaojitokeza. Arusha inafuata ikiwa na ongezeko la kutoka asilimia sita (6) mwaka 2021 hadi **8.13** mwaka 2022. Mbeya ilishuhudia ukuaji kutoka asimilia **2.6** hadi **4.22** kipindi hicho.

- Uvumbuzi na shughuli zinazohusiana nao umechangia uchumi na kuwezesha ajira **89,509** mwaka 2022.
- Pamoja na mafanikio haya, Tanzania inakabiliwa na changamoto zinazokwamisha ukuaji wa shughuli za utafiti na uvumbuzi katika sekta ya TEHAMA.

Miongoni mwa changamoto zinazojitokeza sana ni ukosefu wa mifumo imara na rasmi ya kugharaimia shughuli hizo, na uwekezaji. Hali hii inawafanya wavumbuzi wengi wa kidijiti kutegemea akiba zao binafsi na misaada ya familia.

- Utegemezi kwa washirika wa maendeleo na vyanzo vya fedha visivyo rasmi vinafifisha ukuaji na uvumbuzi. Hii inaonesha dhahiri haja ya kuwa na mifumo imara na ya aina mbalimbali ya uwekezaji ili kuwezesha wajasiriamali na wavumbuzi kutumia kikamilifu uwezo wao, na nguvu zao kitaaluma.
- Changamoto nyingine ni wahusika kushindwa kupata mitaji kutokana na kutokuwa na dhamana za mikopo na masharti ya kupata fedha, na kutokuwepo mipango ya kutosha ya elimu kuhusu uendeshaji wa taasisi na ugharimiaji wa shughuli za ujasiriamali.
- Uhaba wa nyenzo zinazopatikana kwa gharama nafuu kwa utafiti na maendeleo pia unakwamisha uvumbuzi na ubora wa shughuli hizo. Isitoshe, upatikanaji na matumizi ya intaneti ya gharama ndogo pia vinaathiri ukuaji wa uvumbuzi. Hali hii inahitaji juhudi zaidi za serikalki kwenye kuendeleza miundombinu inayowezesha intaneti na kuchochea ukuaji wa mifumo ya kidijiti.

Uzingatiaji wa masharti ya usimamizi pia ni changamoto inayofanyiwa kazi. (Rejea ukurasa 4 kuhusu mipango ya TCRA kuendeleza uvumbuzi).

**Serikali itachukua hatua zifuatazo:**

a. Kuanzisha mfumo imara wa kugharimia utafiti, uvumbuzi na maendeleo ya mifumo na huduma za kidijiti na huduma za TEHAMA kwa ujumla.

b. Kuwezesha na kuendeleza uanzishaji wa vituo vya uvumbuzi kidijiti vinavyolenga kutatua masuala yaliyoko.

c. Kushirikiana na taasisi za utafiti na sekta binafsi kuanzisha maeneo ya TEHAMA kwa ajili ya uvumbuzi na ujasiriamali wa kidijiti. (Rejea ya Mhariri: Serikali inaanzisha utaratibu huo kwenye wilaya sita)

d. Kuendeleza biashara za vitu na bidhaa zinazotokana na uvumbuzi ili kufanikisha ushiriki wa wadau kwenye soko la kidijiti na pia kuzalisha ajira.

e. Kuwezesha utangazaji wa kibiashara na uwekezaji wa mitaji kwenye uvumbuzi wa kidijiti.

f. Kuendeleza uelewa wa masuala ya hakimilki na hataza za uvumbuzi kwa wavumbuzi wa humu nchini.

g. Kuendeleza ushirikiano kati ya taasisi za elimu na wanazuoni, na sekta ya TEHAMA.



*Afisa wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Mhandisi Aneth Kilaja akiwafundisha wanafunzi wasichana walipokuwa wakikamilisha mradi wa ubunifu wa TEHAMA katika siku ya Kimataifa ya TEHAMA. PHOTO: TCRA*

# Vilabu vya Kidijiti Kuongoza Ubunifu Mashuleni

Na Mwandishi wetu

Katika hatua muhimu ya kujenga kizazi chenye umahiri wa kidijitali, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inahimiza uanzishaji wa klabu za kidijiti kwenye taasisi za elimu nchini kote.

Vilabu vya kidijiti ni majukwaa muhimu yanayowapa wanafunzi ujuzi wa teknolojia ya Habari na mawasiliano (TEHAMA). Ujuzi huu ni muhimu kwa maendeleo binafsi na kuongeza ushindani wa kitaifa na kimataifa katika uchumi wa kidijiti unaokua kwa kasi kubwa duniani kote.

Akihutubua jijini Arusha kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wasichana na TEHAMA Aprili mwaka huu, Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia, Mhandisi Maryprisca Mahundi, alieleza kuwa vilabu hivi ni muhimu katika kuchochea ubunifu na uvumbuzi miongoni mwa vijana.

Alisema vilabu hivyo vinajenga na kufanikisha mazingira ambapo akili za vijana zinastawi. Ni viwa-nja vya kuzalisha suluhisho za kiteknolojia kwa changa-moto za kijamii. Vitapanda mbegu za uvumbuzi miongoni mwa vijana wa Kitanzania kuanzia umri mdogo, aliongeza.

Naibu Waziri alifafanua kuwa uelewa wa kidijiti kwenye zama hizi ni sawa na uwezeshaji.

> Uanzishwaji wa vilabu vya kidijiti ni mkakati unaotazama mbali ambao unatarajiwa kubadilisha mfumo wa elimu na kuandaa wanafunzi kwa mustakabali unaotawaliwa na teknolojia za kidijiti.

Kupitia vilabu hivi, wanafunzi watajipatia si tu ujuzi wa TEHAMA bali pia mtazamo wa kutatua changamoto za jamii zetu.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA Dkt. Jabiri Bakari amesema lengo ni kuhakikisha kuwa klabu za kidijiti zinaanzishwa katika kila ngazi ya elimu Tanzania. Mamlaka hiyo kushirikiana na wadau wengine wa elimu na teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kwenye kutelekeza mpango huo, alieleza.

Dkt Bakari amesema TCRA imeanza kampeni nchi nzima kuelimisha wadau na kuhamasisha uanzishwaji wa klabu za kidijiti, kuanzia ngazi ya elimu ya chekechea, msingi, sekondari, vyuo na vyuo vikuu.




*Naibu Waziri wa Habari, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Mhandisi Mary Prisca Mahundi aliyeongozana na Mkurugenzi Mkuu wa TCRA Dkt Jabiri Bakari na viongozi wengine wa sekta ya mawasiliano akiwasikiliza wasichana kutoka Pemba, Zanzibar wakiwasilisha wazo la kibunifu katika maadhimisho ya siku ya kimataifa ya wasichana katika TEHAMA 2024 yaliyofanyika kitaifa mkoani Arusha. PICHA: TCRA*

Aliongeza kwamba mpango huo ni sehemu ya mkakati wa TCRA kuhamasisha ukuaji wa matumizi ya TEHAMA ambazo zinawezesha kutumia mifumo ya kidijitali na programu za TEHAMA katika ngazi zote za matumizi kwenye sekta mbalimbali.

Aidha ameeleza kwamba uanzishwaji wa klabu za kidijiti ni msingi mkuu wa kuwezesha ubunifu wa ndani Tanzania na uvumbuzi unaolenga kutatua changamoto za maeneo husika.

Kampeni inayoendelea inatekelezwa kupitia ofisi ya TCRA Zanzibar na ofisi za kanda. TCRA ina ofisi kwenye kanda tano – Mashariki (Dar es Salaam), Ziwa (Mwanza), Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), Kati (Dodoma) na Kaskazini (Arusha).

Klabu hizi zinawezesha vijana wa Kitanzania kupata stadi zinazohitajika ili kushiriki uchumi wa kidijiti. zinaundwa kwenye ngazi zote za elimu na zitakuwa majukwaa muhimu ya kielimu yatakayozalisha wavumbuzi na viongozi wapya kwenye teknolojia.

> “
>
> Mwongozo wa TCRA wa uanzishaji wa klabu, unazielezea klabu hizi kama majukwaa kwenye taasisi za elimu yatayowapatia watoto na wanafunzi kuanzia chekechea hadi vyuo vikuu stadi za kidijiti wanazohitaji kufanikiwa kwenye uchumi wa kidijiti.
>
> — Dr Jabiri Kuwe Bakari
>
> *TCRA Director General*




Mpango huo pia unaenda sambamba na hatua za kuendeleza masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati na pia kuimarisha fikra za wanafunzi na uwezo wao wa kuvumbua.

Mhandisi Imelda amefafanua kuwa klabu hizo ziko wazi kwa wanafunzi wote na sio tu wale wanaochukua masomo hayo. Kila mwanafunzi anaweza kushiriki kwenye klabu hizo, amesema.

Uanzishaji, uendeshaji na uendelevu wa klabu hizi unahitaji juhudi za ushirikiano wa wadau mbalimbali. Hao ni pamoja na taasisi za elimu, wanafunzi, wazazi na walezi na jamii kwa ujumla.

Shule zitatoa na kuwezesha kutumika miundombinu, raslimali na teknolojia, wakati wazazi na jamii wanategemewa kuunga mkono na kuhimiza vijana kuanzisha na kujiunga na klabu hizi.

TCRA imechapisha taarifa kuhusu utaratibu kwa wanaopenda kuanzisha klabu za kidijiti. Wanaweza kujisajili kwenye tovuti maalum ya mpango huo, ambayo ni: digitalclubs.tz.

Taarifa zaidi zinapatikana kwa kupiga simu ya bure, namba

**0800008272**

DONDOO ZA USALAMA MTANDAONI

# Kujilinda Dhidi ya Meseji za Ulaghai

Katika enzi hii ya kidijitali, simu janja ni zana muhimu inayorahisisha mawasiliano, lakini pia imekuwa njia moja wapo inayotumiwa na matapeli mtandaoni. Ili kuepuka utapeli kwa njia ya ujumbe mfupi.

## Zingatia yafuatayo:

### Jielimishe:

Maarifa ni kinga yako ya kwanza. Jitahidi kujifunza mbinu mbalimbali za utapeli unaofanyika kupitia SMS. Matapeli mara nyingi hutumia mbinu za kukushawishi kwa ahadi za zawadi kubwa au kuhimiza utoaji wa taarifa binafsi. Kuwa makini na usishirikishe taarifa zako binafsi na mtu yeyote usiyemfahamu vyema.

### Hakiki mtumaji wa ujumbe mfupi:

Daima chukua tahadhari unapopokea ujumbe mfupi au simu kutoka kwa namba usiyoifahamu. Iwapo ujumbe unaonekana kuwa wa kutiliwa shaka au una vishawishi vikubwa, uwezekano mkubwa ni utapeli. Endapo unapata shaka, ni bora kuwa makini zaidi.

### Ripoti matukio ya ulaghai:

Ikiwa utapokea ujumbe unaoshukiwa kuwa wa kitapeli, ripoti mara moja kwa kutuma neno “utapeli” kisha weka namba ya mtumaji kwenda 15040. Mamlaka husika zitachukua hatua.

### Mawasiliano rasmi na mtoa huduma:

Unapohitaji kuwasiliana na mtoa huduma wako wa simu, tumia namba rasmi pekee, ambayo ni “100”. Epuka kutoa ushirikiano kwa namba nyingine yoyote na ufuate maelekezo ya namba hiyo pekee.

### Linda taarifa zako za kibinafsi:

Epuka kushirikisha taarifa zako nyeti mtandaoni, kama vile maelezo ya kadi yako ya simu au ya kibenki. Kutoa taarifa hizo kunaweza kurahisisha utapeli. Chukua tahadhari unapoweka taarifa zako binafsi kwenye mitandao ya kijamii.




### Fanya Sasisho la Mfumo wa Uendeshaji:

Kuhakikisha mfumo wako wa uendeshaji wa kifaa cha mawasiliano umesasishwa ni muhimu, kwani sasisho hizi zinaboresha ulinzi wa kifaa chako.

### Kuwa mwangalifu

Wahalifu mtandaoni mara nyingi wanatumia njia na mbinu mbalimbali za kukuhadaa na kujenga imani yako kwao. Wanaweza kujifanya kuwa wanawakilisha watoa huduma husika au kuja na mipango inayotamanisha. Tukumbuke kwamba watoa huduma wenye leseni hawatafuti taarifa zako za binafsi na zinazohusu masuala yako ya kifedha kupitia meseji au simu za maongezi.

Wakati wote ukiwa na mashaka na anayewasiliana nawe, kata simu na mpigie mtoa huduma wako moja kwa moja kutumia namba rasmi ya huduma kwa wateja, kama vile 100.

### Sambaza maarifa

Kumbuka, usalama mtandaoni ni jukumu letu sote. Tujilinde na tuwalinde wapendwa wetu dhidi ya matapeli mtandaoni.

MAREJEO YA SHERIA/KANUNI ZA SEKTA

# Kanuni za Utangazaji wa Jamii 2023

Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta za Kusimamia Huduma za Utangazaji za Jamii za mwaka 2023 zinatoa mwongozo muhimu wa uendeshaji wa huduma za utangazaji wa jamii Tanzania Bara. Kanuni hizi zimeundwa kwa Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Sura ya 306) na zilianza kutekelezwa rasmi tarehe 25 Agosti, 2023.



## Baadhi ya masuala yanayobainishwa kwenye Kanuni hizi ni:

**Utoaji Leseni:**

Kanuni zinaweka wazi taratibu za kuhakikisha kuwa leseni za uendeshaji wa vituo vya utangazaji wa jamii zinatolewa kwa uwazi na haki. Hii inahakikisha kuwa vituo vyote vinavyofanya kazi vinafuata viwango vya sheria na kanuni za sekta zilizopo na vinachangia katika maendeleo.

**Umiliki na Uendeshaji:**

Vituo vya utangazaji wa jamii vinatakiwa kutokuwawa vya kibiashara. Vilevile vinatakiwa kumilikiwa na kuendeshwa hasa na taasisi za elimu, mamlaka za serikali za mitaa, vilabu vya kijamii, mashirika yasiyo ya kiserikali, na vikundi vingine vya kijamii. Vyama vya siasa, watu binafsi, taasisi za dini, makampuni ya kibiashara, na makundi mengine yasiyo na uhusiano yanakatazwa kumiliki huduma za utangazaji wa jamii.

**Kuchochea Ushiriki wa Jamii:**

Moja ya malengo makuu ya kanuni hizi ni kuchochea ushiriki wa jamii katika shughuli za maendeleo. Utangazaji wa jamii unatambuliwa kama chombo cha kuwezesha sauti za wale wasiosikika mara kwa mara na kuimarisha uwezo wa jamii kushiriki katika kujadili na kushughulikia masuala yao ya ndani.

**Kuimarisha Maudhui ya Ndani:**

Kanuni zinasisitiza umuhimu wa maudhui ya ndani katika utangazaji wa jamii. Hii inalenga kuhamasisha utengenezaji na usambazaji wa vipindi vinavyoakisi utamaduni, mila na masuala yanayogusa maisha ya watu wa eneo husika, hivyo kusaidia kukuza utambulisho wa kitaifa na kikanda.

**Miongozo ya Maudhui:**

Vipindi lazima viangazie mahitaji na malengo ya jamii husika, pamoja na elimu, afya, maendeleo ya kiuchumi na utajirishaji wa utamaduni. Angalau asilimia 80 ya maudhui ya utangazaji yanapaswa kushirikisha jamii ya mahali ambapo kituo kimeanzishwa.

**Maudhui Yaliyokatazwa:**

Kanuni zinakataza vikali utangazaji unaokiuka maadili, unaodhoofisha uadilifu, unaohamasisha ubaguzi au vurugu, unaoeneza maudhui ya kingono au ponografia na unaodharau shughuli za Serikali, Bunge au Mahakama.

**Vyanzo vya Mapato:**

Vituo vya utangazaji wa jamii vinaweza kufadhili operesheni zao kupitia michango, ruzuku, matangazo ya kijamii na ushirikiano na mashirika yaliyoidhinishwa ya maendeleo.

**Kanuni hizi zinaweka msingi imara unaohakikisha ufikishaji wa huduma za utangazaji kwa maeneo mengi zaidi Tanzania Bara, ikiwemo maeneo ya mpakani.**

TAKWIMU

# Upimaji viwango vya mawasiliano waonesha tija

Na Peter Lyimo


Watoa huduma za mawasiliano Tanzania wamefikia viwango vya ubora wa huduma vilivyowekwa, ripoti ya mwenendo wa sekta ya mawasiliano ya Juni 2024 inaonesha.

Ripoti hiyo, iliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa TCRA Dkt. Jabiri Bakari inatokana na

durusi ya ubora wa huduma kwenye maeneo 14 yanayohusu mitandao Aprili na Juni 2024

Watoa huduma za mawasiliano watano ambao ni Airtel, Halotel, Tigo, TTCL na Vodacom walifanyiwa tathmini.

Durusi pia iliangazia maendeleo katika teknolojia za simu za uzao wa pili (2G), wa tatu (3G), wa nne (4G) na wa tano (5G). Uzao wa pili unawezesha maongezi na ujumbe mfupi, 3G unawezesha vyote hivi maoja na huduma za intaneti na data, 4G una sifa za uzao wa tatu na unawahakikishia watumiaji wake intaneti ya kasi. Uzao wa tano unawezesha upatikanaji na matumizi ya intaneti ya kasi kubwa na yenye ubora wa juu.






Ufikiaji wa huduma za 3G umeongezeka kutoka asilimia 88 hadi 89, na 4G kutoka asilimia 80 hadi 83. Ufikiaji wa teknolojia ya 5G, iliyoingia nchini mwaka 2022, umefikia asilimia 13 – kuoka 12 Machi 2024.

Upimaji wa viwango vya ubora wa huduma za mawasiliano hufanyika mara kwa mara, ambapo matokeo yatokanayo na upimaji yanayofanywa na TCRA pamoja na watoa huduma huchambuliwa kwa ushirikiano wa karibu.

Hii ni kuhakikisha kwamba huduma za mawasiliano zinazotolewa zinakidhi viwango vya ubora vinavyotakiwa.

Mawasiliano miongoni mwa mashine yaimarika Tanzania.

Teknolojia ya mawasiliano baina ya vifaa vinavyojiendesha vyenyewe bila ushiriki wa binadamu inakua Tanzania, ambapo laini za simu kwa matumizi ya mashine kwa mashine zimeongezeka kwa asilimia 4.3 ndani ya miezi mitatu, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt Jabiri Bakari amesema.

Teknolojia hii, inayojulikana kwa kifupisho cha lugha ya Kiingereza kama M2M inawezesha vifaa kuwasiliana yenyewe na kubadilishana data na taarifa bila ushiriki wa binadamu. Kulikuwa na laini 962,928 zilizotumiwa na mashine Juni 2024 kulinganisha na 937,257 Aprili mwaka huu, takwimu za hali ya mawasiliano Tsnzania zinaonesha.

Mifano ya teknolojia hiyo ni mita za kisasa za umeme na matumizi ya nishati, kamera za usalama wa maeneo ambavyo vinaweza kutuma taarifa kwenye simu ya mkononi ya mmilki akiwa mbali. Hii inamwezesha kufuatilia matumizi na matukio muda wote akiwa mbali.

Matumizi mengine ni kwenye mifumo wa usambazaji wa bidhaa ambapo majokofu ya kisasa yanaweza kuagiza vitu kwenye maduka kadri vinavyopungua.


Teknolojia pia inatumiwa kwenye vifaa vinavyovaliwa na wahusika, mithinli ya saa za mkononi, ili kufuatilia afya, ukakamavu na shughuli za kila siku za mhusika. Vinahamisha taarifa kwenye vyombo vingine kama vile simu janja na kompyuta zilizounganishwa kwenye mitandao. Taarifa ya TCRA zinaonesha kwamba vifaa vye kuvaa mwilini 7,721 vilikuwa vinatumika Tanzania Juni 2024.

Takwimu hizo pia zinaonesha kuwa gharama za vifurushi au bando kwa data zimeshuka kwa asilimia 0.6 kati ya Aprili na Juni. Dkt Bakari ameeleza kuwa wastani wa gharama za maongezi kwenye mtandao wa mtumiaji na kwenda mitandao mingine zilianza kukaribiana mwaka 2020 kufuatia kushuka kidogo kidogo miaka iliyotangulia.

Gharama za maongezi kwenye mtandao wa mtumiaji zilishuka kutoka shilingi 149 kwa dakika mwaka 2019 hadi shilingi 26 Juni 2024. Gharama kwenda mitandao mingine zilishuka kutoka shilingi 189 kwa dakika hadi shilingi 28.

Kiwango cha kila mwaka cha ukuaji wa simu za maongezi kwenda mitandao mingine kilikuwa mara saba ya kile cha simu ndani ya mtandao wa mtumiaji kati mwaka 2019 na 2023.

Wakati simu ndani ya mtandao ziliongezeka kwa asilimia tisa (9) kwa mwaka kipindi hicho, simu za watumiaji kwenda mitandao mingine zilipaa kwa asilimia 61.



Taarifa inaeleza kuwa kushuka kwa gharama za simu kwenda mitandao mingine kumesababishwa na kuchangiwa na kupunguzwa kwa gharama za kuunganisha simu baina ya mitandao kipindi hicho. Gharama za kuunganisha zimeshuka kutoka shilingi 15.6 Januari 2018 hadi 1.76 Januari 2024.

Taarifa pia inaonesha kuwa asilimia 56 ya watu Tanzania wanapata huduma za utangazaji wa televisheni kidijitali kwa mifumo ya ardhini, ambao umeenea kijiografia nchini kwa asilimia 32. Matangazo ya redio kwa masafa ya FM yanafika asilimia 49.94 ya eneo la Tanzania. Aidha huduma za redio za FM zinapatikana kwa asilimia 75.52 ya watu nchini.

Maudhui ya utangazaji Tanzania yanatolewa kwa redio, televisheni za kidijitali mifumo ya ardhini na setilaiti na kwa waya. Vilevile yanapatikana kupitia vyombo vya mitandaoni, yaani redio na televisheni mtandaoni na blogu.

TCRA imetoa leseni mpya 24 za huduma mbalimbali za utangazaji kati ya Aprili na Juni mwaka huu.

Hizo ni pamoja na redio nane (8) za wilaya, televisheni tisa (9) za kitaifa za kulipia,na redio mtandao mbili. Nyingine ni leseni mbili za waandaaji na watayarishaji maudhui na tatu za televisheni kwa njia ya waya.

Hadi Juni 2024 kulikuwa na televisheni za kitaifa zisizolipiwa 26 na televisheni zisizolipiwa za wilaya 23. Vilevile kuna redio za kitaifa 14, za ngazi ya mkoa 31 na za wilaya 17.

Nyingine ni redio za jamii 25, televisheni za taifa za kulipia 25 na televisheni ya kulipia ngazi ya wilaya moja (1).

Leseni tano (5) zimetolewa kwa watayarishaji na waandaji wa maudhui, blogu 64, redio mtandaoni tisa, televisheni mtandaoni 215 na televisheni kwa waya 63.

Wakati huo huo TCRA imetoa leseni mpya 12 kwa watoa huduma za usafirishaji wa vifurushi kati ya Aprili na Juni mwaka huu. Hatua hii inaonesha mikakati ya kuendeleza usafirishaji vifurushi ambao ni muhimu kwenye biashaaa mtandao.

Leseni sita (6) zimetolewa kwa wasafirishaji kati ya miji (6). Wengi wao ni wanaotoa huduma za mabasi ya abiria. Nyingine ni kwa watoa huduma ndani ya mji mmoja husika (tatu), usafirishaji virurushi Afrika Mashariki (moja), usafirishaji vifurushi kimataifa (mbili).

Hadi Juni 2024 kulikuwa na watoa huduma za usafirishaji vifurushi kati ya miji 71, wasafirishaji ndani ya nchi 46 na watoa huduma ndani ya mji mmoja 18. Wengine ni usafirishaji vifurushi Afrika Maskariki wawili na wa kimataifa wananе.

TAKWIMU

# Mikoa ya Zanzibar yapaa kimawasiliano

Laini za simu za mkononi zilizosajiliwa mkoa wa Kaskazini Pemba zimeenea miongoni mwa watu kwa asilimia 125 wakati mkoa wa Mjini Magharibi ni wa tatu Tanzania nzima kwa kuwa na minara yenye vifaa vya kuwezesha mawasiliano ya simu za mkononi uzao wa tano (5G), kwa mujibu wa ripoti rasmi.

Taarifa ya hali ya mawasiliano Tanzania kati ya Aprili na Juni 2024 inaonesha usajili laini za simu umeongezeka Pemba Kaskazini kutoka asilimia 100 Septemba 2022 hadi 124 Aprili mwaka huu.

Kwa ujumla laini za simu Unguja na Pemba zime ongezeka kwa asilimia 45 kati ya Septemba 2022 na Juni 2024.

Laini mkoani Kaskazini Pemba zimeongezeka kutoka 94,594 zilizosajiliwa huko Septemba 2022, na ambazo zilienea miongoni mwa wananchi kwa asilimia100, hadi laini 118,329 zilizoenea kwa asilimia 125 Kaskazini



Pemba sasa ni ya 10 Tanzania nzima kwa asilimia ya kuenea laini miongoni mwa wananchi.

Mkoa huo ulikuwa wa tisa Tanzania nzima Septemba 2022. Hata hivyo, mkoa wa Kaskazini Unguja bado ni wa mwisho Tanzania nzima kwa kuenea kwa laini miongoni mwa wananchi.

Mikoa iliyoongeza nafasi za usajili kitaifa ni Kilimanjaro iliyotoka nafasi ya sita hadi ya nne, Mwanza (nane hadi saba), Dodoma (10 hadi nane), Pwani (16 hadi 11), Ruvuma (18 hadi 15 na Simiyu (24 hadi 22).

Mikoa iliyoshuka ni Njombe (nne hadi sita), Mtwara (saba hadi tisa), Morogoro (11 hadi 12), Mara (25 hadi 26) na Tabora 13 hadi 16).

Mikoa iliyobakiza nafazi zake za juu ni pamoja na Dar es Salaam (1), Arusha (2) na Mbeya (3). Iliyobakia chini ni Kigoma (27) Kusini Pemba (30) na Kusini Unguja (31)

### Jedwali 1: Mikoa mitano inayoongoza kuwa na minara mingi yenye vifaa vya uzao wa tano (5G) Tanzania

| Nafasi Kitaifa | Mkoa/Eneo | Minara ya 5G |
|---|---|---|
| 1 | Dar es salaam | 541 |
| 2 | Dodoma | 41 |
| 3 | Mjini Magharibi | 37 |
| 4 | Arusha | 27 |
| 5 | Mwanza | 23 |

### Jedwali 2: Ongezeko la laini la simu kati ya Septemba 2022 na Juni 2024

| Mkoa | Septemba 2022 | Juni 2024 | Ongezeko | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Mikoa ya Unguja | 428,873 | 660,114 | 231,241 | 54 |
| Mikoa ya Pemba | 189,916 | 236,457 | 46,541 | 25 |
| Mikoa yote Zanzibar | 618,789 | 896,571 | 277,784 | 45 |
| Mikoa yote Tanzania | 58,032,985 | 76,550,934 | 18,517,949 | 32 |
| Mikoa yote Tanzania Bara | 57,414,196 | 75,654,363 | 18,240,167 | 32 |

# UTARATIBU WA UTOAJI LESENI ZA POSTA NA USAFIRISHAJI VIFURUSHI

Utoaji leseni unalenga kuendeleza ushindani wenye tija miongoni mwa watoa huduma. Ufanisi huu unawawezesha watumiaji kupata huduma zenye ubora na kwa gharama nafuu.

Huduma za usafirishaji vifurushi ni shughuli maalum zinazohusu ukusanyaji, usafirishaji na ufikishaji vitu vinavyopita mfumo wa kiposta, isipokuwa barua. Vitu vinavyosafirishwa na watoa huduma wenye leseni za kundi hili ni nyaraka, vifurushi na vipeto, ambavyo kwa kawaida vinatakiwa kufikishwa haraka kwa walengwa.

Ukusanyaji, usafirishaji na ufikishaji wa barua unafanywa na mtoa huduma wa shughuli za posta wa umma mwenye ukiritimba katika shughuli hii. Kwa Tanzania ni Shirika la Posta Tanzania (TPC). Usafirishaji vifurushi umeachiwa watoa huduma wote wenye sifa, ambao wanashindana.

Kuna aina tano ya leseni za usafirishaji vifurushi zinazotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). Hizo ni kwa usadfirishaji ndani ya nchi na usafirishaji kati ya miji, ambamo nyingi ni kwa wanaotoa pia huduma za mabasi ya abiria. Nyingine ni kutoa huduma ndani ya mji mmoja husika, usafirishaji Afrika Mashariki na kimataifa.

Leseni zinatolewa kwa kampuni za usafirishaji wa vifurushi, wakala wa mizigo na kampuni za usafiri na usafirishaji baada ya kuwasilisha maombi kupitia mfumo wa maombi mtandaoni wa: https://tanzanite.tcra.go.tz/index.htm.




## Aina na soko la leseni, ada na muda wa leseni

| Aina ya leseni | Ada (Shilingi) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Maombi | Ada ya awali | Ada ya kuhuisha | Ada ya mwaka | Muda wa leseni (miaka) |
| Mtoa huduma za Posta wa Umma | 2,300,000 | 20,000,000 | 20,000,000 | 20,000,000 | 25 |
| Usafirishaji Kimataifa | 170,000 | 18,000,000 | 170,000 | 18,000,000 | 5 |
| Usafirishaji Afrika Mashariki | 100,000 | 6,000,000 | 100,0000 | 6,000,000 | 3 |
| Usafirishaji ndani ya nchi | 60,000 | 3,000,000 | 60,000 | 3,000,000 | 3 |
| Usafirishaji ndani ya mji | 60,000 | 1,400,000 | 60,000 | 1,400,000 | 3 |
| Wasafirishaji kati ya miji | 60,000 | 400,000 | 60,000 | 400,000 | 3 |

## Ada ya postikodi kwa shughuli au matukio maalum (Kwa shilingi)

| Maombi | Ada ya awali | Ada ya kuhuisha | Muda wa leseni (miaka) |
|---|---|---|---|
| 10,000 | 100,000 | 100,000 | Siku 30 |

# Takwimu za Mawasiliano katika namba

## Takwimu za Mawasiliano ya Simu

Sehemu hii inahusika na laini za simu za mkononi na za mezani ambazo zimetumika angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu iliyotangulia


Kuna aina mbili za laini: zinazotumika kwa mawasiliano ya binadamu (Person to Person - P2P) na zinazotumika kwa mawasiliano ya mashine kwa mashine (M2M)

**Watumiaji wa laini za zimu wamekuwa wakiongezeka kila robo muhula**


| Machi 2024 | Juni 2024 | |
|---|---|---|
| Milioni 73.4 | Milioni 76.6 | 4.3% |

## Mgawanyo wa usajili wa laini kwa kila mtoa huduma

### Watumiaji wa P2P





### Watumiaji wa M2M




## Kuelekea uchumi usio wa fedha taslimu: Jinsi gani watumiaji wa pesa mtandao wameongezeka

**Watumiaji wapya milioni 2, wa pesa mtandao wameongezeka ndani ya robo muhula**





5%

**Zaidi ya 89% ya soko la pesa** mtandao linatawaliwa na **Tigo Pesa, M-Pesa, na Airtel money.**

### Miamala ya fedha mtandao

| Machi 2024 | Juni 2024 |
|---|---|
| 473,163,645 | 295,925,437 |

### Watumiaji wa pesa mtandao



# Takwimu za matumizi ya huduma ya Intaneti

Milioni **36.8**
Machi 2024

Milioni **39.3**
Juni 2024

Idadi ya laini za Intaneti imeongezeka kwa 7% kutoka milioni 36.8 kwa robo ya mwaka iliyoishia Machi 2024 hadi milioni 39.3 kwa robo ya mwaka iliyoishia Juni 2024

**7%**

## Idadi ya laini zinazotumia Intaneti kwa kila mwezi katika robo ya mwaka inayoishia Juni 2024

Huduma ya intaneti kwa simu ndiyo inatumika zaidi kulinganisha na intaneti nyingine mpaka Juni 2024, ilikuwa na **99.6%** ya watumiaji wote

**99.6%**

| Mwezi | Huduma ya intaneti kwa simu | Fixed wireless | Fixed wired | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Aprili | 37,189,561 | 56,311 | 35,126 | 37,280,998 |
| Mei | 38,152,800 | 60,328 | 34,865 | 38,247,993 |
| Juni | 39,214,908 | 56,130 | 40,439 | 39,311,477 |

# Takwimu za Huduma za Utangazaji

**milioni 3.84**
Jumla ya visimbuzi vilivyopo, vilivyo hai na visivyo hai

**milioni 1.6**
Jumla ya visimbuzi vilivyo hai

**79%**
ya visimbuzi hai milioni 1.6 ni aina ya DTH,yaani satelaiti

## Idadi ya visimbuzi vinavyotumika kwa kila mtoa huduma

| Mtoa huduma DTT (mitambo ya ardhini) | DTT (satelaiti) | DTH | Jumla |
|---|---|---|---|
| Agape Associates Limited | 1,840 | 0 | **1,840** |
| Azam Media Limited | 206,527 | 863,176 | **1,069,703** |
| Basic Trasmission Limited (Digitek) | 15,000 | 0 | **15,000** |
| Basic Trasmission Limited (Continental) | 38,020 | 30,842 | **68,862** |
| Multichoice Tanzania Limited (DSTv) | 0 | 233,607 | **233,607** |
| Star Media Limited | 79,502 | 98,329 | **177,831** |
| Zuku | 0 | 23,106 | **23,106** |
| **Jumla** | **340,889** | **1,249,060** | **1,589,949** |